# UTAFITI SHIRIKISHI

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

FOSTA HEALTH

GCRFAFRICAP
CLIMATE SMART AGRICULTURAL DEVELOPMENT

Centre for Climate Change Economics and Policy
An ESRC Research Centre

**MRADI ULIYOFANYWA NA CCCEP | MUHTASARI NAMBA 5 | SEPTEMBA 2024**



## UTAFITI SHIRIKISHI NI NINI?

Wakati maamuzi muhimu yanapofanywa kuhusu masuala ya kijamii, ni muhimu kuzingatia ni nani mwenye nguvu na ni nani anaye weza kuzungumza na kusikika.

Utafiti shirikishi ni mbinu ya ubora inayochunguza masuala ya kijamii kupitia ushirikiano wa moja kwa moja na makundi yaliyoathiriwa. Inatambua kwamba mitazamo ya kijamii na vipaumbele vya wananchi wa eneo husika ni muhimu katika usimamizi wa masuala ya kijamii.

Utafiti shirikishi mara nyingi hutumia mbinu na zana ambazo zinaweza kufanyika kwa njia ya kushirikisha na kidemokrasia – ikiwapa sauti na uchaguzi watu walioathirika katika jinsi maisha yao na mazingira yao yanavyosimamiwa. Mbinu hizi zinaweza kuwa kwa njia ya mazungumzo, picha, au za ubunifu. Hii inaweza kuwa na manufaa hasa katika kuwashirikisha makundi yaliyotengwa ndani ya mchakato wa utafiti.

VIWANGO VYA USHIRIKISHWAJI

Ushirikishaji unaweza kufikiriwa kama ngazi – kulingana na kiwango cha ushirikishaji kilichofikiwa ndani ya mchakato wa utafiti na utekelezaji.

Kutoshirikishwa ni kuunda bodi za ushauri ambazo katika utekelezaji hazina nguvu kubwa na zinawapotosha wananchi kwa kuwadanganya.

Kuwajulisha au kuwashirikisha tu wananchi walioathirika kuhusu muundo wa miradi na sera bila kujumuisha mitazamo yao kunachukuliwa kama uhusiano wa kishirika tu. Ili kukuza umiliki na uwezeshaji miongoni mwa wananchi walioathirika, tunapaswa kuwaruhusu waongoze mchakato kadri inavyowezekana kupitia ushirikiano wa haki.

Ushiriki kama udhibiti wa raia huwezesha na kuwapa uwezo watu walioathiriwa kuwa wasimamizi wa masuala yanayowahusu.

Ni muhimu kuhakikisha ushirikishwaji wa jamii zilizoathirika katika kubuni, utekelezaji, na tathmini ya utafiti na utekelezaji, kwani zina uzoefu wa kipekee na muhimu kuhusu shughuli za mradi.


### FAIDA ZA MBINU SHIRIKISHI

**1** Inatambua kwamba jamii zilizoathirika mara nyingi ziko katika nafasi bora ya kuelewa na kusimamia mazingira yao

**2** Inawapa jamii zilizoathirika sauti katika maeneo ambayo mara nyingi hazizingatiwi – kwa mfano, kubuni miradi na kutengeneza sera

**3** Jamii zilizoathirika zinashirikishwa zaidi na kuwekeza katika shughuli za mradi kwa kuwa wanajiona kuwa ni sehemu ya mradi na unalingana na matarajio yao

**4** Inasaidia mradi kuwa endelevu kwa kuwa jamii zilizoathirika zinaweza kuendeleza shughuli za mradi baada muda wa mradi kukamailika




Arnstein's Ladder (1969)
Degrees of Citizen Participatio

## MBINU ZA USHIRIKISHWA: FOSTA – AFYA & SAUTI YA PICHA

Hapa Tanzania, FoSTA-Health inatumia mbinu ya ushirikishaji ya SAUTI YA PICHA (Photovoice) kuchunguza mienendo ya kijinsia na shughuli za kilimo katika Milima ya Usambara Mashariki, mkoani Tanga.

SAUTI YA PICHA ni mbinu ya ubunifu ya ushirikishaji kwa vitendo, kwa kuona na kujadili picha mbalimbali zilizopigwa na washiriki. Picha hizi zina lenga Maisha yao ya kila siku na wanazitumia kutoa hadidhi mbalimbali kulingana na matukio ya picha yeneyewe.

Lengo kuu la FoSTA-Health ni kuruhusu 'washiriki' kuongoza mchakato wa utafiti kadri inavyowezekana. Kundi linadhibiti nini kipigwe picha na nani wakuonyeshwa  picha hizo.



*"Katika warsha, napenda jinsi nilivyopata ujasiri wa kuzungumza mbele ya watu wengi. Sijawahi kuzungumza mbele ya watu wengi, lakini siku hiyo nilienda mbele kuelezea picha, hivyo nilipata ujasiri wa kuzungumza na watu... hata kama mara nyingine nitakaribishwa sehemu nyingine kama Muheza kwa warsha nyingine, nina ujasiri wa kukutana na watu hao na nina uzoefu wa kujibu maswali."* – Mshiriki wa Sauti ya Picha

## KUSHIRIKIANA KUUNDA AJENDA

Katika FoSTA-Health, tumelenga kuingiza ushirikishaji katika mchakato mzima wa SAUTI YA PICHA. Sehemu muhimu ya hili ilikuwa kushirikiana kuunda mpango kati ya mtafiti na 'washiriki' wakati wa mikutano ya awali. Hii ilihusisha kuuliza kundi kuhusu: a) matarajio yao ya ushirikishaji, b) faida wanazotarajia kupata kutokana na kushiriki, c) picha wanazotaka kupiga, d) nani wangependa kuwaonyesha picha hizo, na e) kuchunguza changamoto zao zinazohusiana na ushiriki na kufikiria njia za kuzitatua.

Mchakato huu umeweza kuhakikisha kwamba washiriki wanahisi mitazamo yao inathaminiwa na ni ya muhimu, jambo ambalo limeimarisha mahusiano na kuleta uaminifu kati ya washiriki na watafiti.

Kuwaruhusu washiriki kushiriki hadithi zao na uzoefu wa maisha kupitia picha kumewezesha kundi hilo kutambua changamoto za pamoja zilizopo ndani ya jamii zao katika Hifadhi ya Mazingira Asili ya Amani – iliyoko Wilaya ya Muheza, Milima ya Usambara Mashariki, Tanzania. Kushirikisha changamoto hizi na watunga sera na wataalamu wakati wa maonyesho ya SAUTI YA PICHA kumeipa kundi hilo ujasiri wa kueleza mabadiliko wanayotarajia kuona.

# MAPENDEKEZO

- Mbinu za ushirikishaji zinaweza kusaidia kuoanisha nadharia ya mabadiliko ya mradi na matarajio ya mtu binafsi na jamii kwa kuwaleta watu hawa pamoja na uzoefu wao wa kipekee, mahitaji, na matamanio katika mchakato wa kutengeneza sera na utekelezaji.
- Lenga kushirikiana katika kubuni malengo ya mradi na hatua za utekelezaji pamoja na jamii walioathirika ili kuhakikisha wanahusika  katika utekelezaji wa  mradi tangu mwanzo.
- Fikiria kutumia mbinu tofauti na za ubunifu katika kubuni, kutekeleza, na kufuatilia mradi kama njia ya kuwawezesha jamii na kuwapa sauti, huku ukiepuka ushirikiano wa kishirika (tokenistic) na kuelekea udhibiti wa raia (citizen control).
- Kusikiliza na kujumuisha mitazamo ya jamii kunaweza kuleta uendelevu wa shughuli za mrada hata baada ya kipindi cha mradi kumalizika, kwani wanajamii wanahisi kuwa na udhibiti mradi husika.










Prepared and disseminated through collaboration with the ESRC Climate Change Centre for Economics and Policy Legacy project led by UoLeeds and Tanzania Forest Conservation Group

Tanzania Forest Conservation Group
Centre for Climate Change Economics and Policy
An ESRC Research Centre

To find out more about the project, please visit fosta-health.eu

FOSTA HEALTH